FUNZO LA 7

1. Ulimwengu ulikuwa namna gani kabla ya Mungu kuumba?
-Hapo mwanzo, hapakuwa na mwangaza.
-Hapo mwanzo, giza lilizingira dunia nzima.

2. Mungu aliumbaje nuru siku ya kwanza?
-Mungu aliumba nuru kwa kunena tu.

3. Mungu aliumbaje mbingu siku ya pili?
-Mungu aliumba mbingu kwa kunena tu.

4. Mungu alitenganishaje maji yaliyozingira nchi?
-Mungu aliyaweka maji mengine kutoka kwa nchi juu ya mbingu.
-Mungu aliyaacha maji yaliyobaki juu ya nchi.

5. Nani aliyaagiza maji yakusanyike ili kuwe na nchi kavu?
-Mungu.

6. Kwa nini Mungu anaweza kuagiza maji kukusanyika mahali na yakamtii?
-Kwa sababu Mungu ndiye muumba wa maji.

7. Mungu aliumbaje mimea na miti yote?
-Mungu aliumba mimea na miti yote kwa kunena tu.

8. Mungu aliumba mimea na miti yote ili isaidie nani?
-Mungu aliumba mimea na miti yote isaidie binadamu.



9. Kwa nini Mungu aliumba mimea na miti yote?
-Kwa sababu Mungu anatupenda sana.

10. Mungu aliumbaje jua, mwezi na nyota?
-Mungu aliumba jua, mwezi na nyota kwa kunena tu.

11. Mungu aliumbaje samaki na ndege wote?
-Mungu aliumba samaki na ndege wote kwa kunena tu.

12. Mungu aliumba samaki na ndege wote kusaidia nani?
-Mungu aliumba samaki na ndege kusaidia binadamu.

13. Kwa nini Mungu aliumba samaki na ndege wote?
-Kwa sababu Mungu anatupenda sana.

14. Mungu alisema nini kuhusu vyote alivyoumba?
-Mungu alisema kuwa kila kitu ni kizuri.

15. Kwa nini Mungu aliweza kuumba kila kitu kikamilifu?
-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.

-Mungu aliumba nini siku ya sita?

Tusome Mwanzo 1:24-25

24-Mungu akasema, “Nchi na itoe aina zote za viumbe hai, wanyama wa kufugwa, viumbe vitambaavyo na wanyama wa porini wa kila aina.” Ikawa hivyo.
25-Basi, Mungu akafanya aina zote za wanyama wa porini, wanyama wa kufugwa, na viumbe vitambaavyo.

-Siku ya sita Mungu aliwaumba wanyama wote.

-Mungu aliumba wanyama aina ngapi?
-Wengi ambao hawawezi kuhesabika.

-Nani pekee ambaye aliweza kuumba wanyama?

-Mungu pekee.
-Mungu pekee anayeweza kuumba wanyama.

-Mungu alipomaliza kuwaumba wanyama, nchi ilikuwa imetayarishwa.

-Je, Mungu alitayarisha nchi kwa malaika au kwa Shetani na mapepo wake?
-La.

-Mungu alitayarishia nani nchi?
-Mungu alitutayarishia nchi sisi wanadamu.

-Mungu alitayarishia binadamu nchi kamilifu kwa sababu anatupenda sana.

-Mungu hakutayarishia malaika nchi.
-Mungu hakutayarishia mapepo nchi.
-Mungu hakutayarishia Shetani nchi.

-Mungu alitutayarishia sisi binadamu pekee nchi.

-Tusome Mungu alichosema baada ya kututayarisha nchi:



Tusome Mwanzo 1:26

26-Kisha Mungu akasema, “Tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; atawale samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa kufugwa, dunia yote na viumbe vyote vitambaavyo.”

-Mungu akasema, “Wacha tumuumbe mtu kwa mfano wetu.”

-Mungu alikuwa anamwongelesha nani?

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu walikuwa wakiongea pamoja.

-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu walikuwa wakiongea kuhusu kutuumba sisi binadamu kwa mfano wao.

-Kwa kila kitu alichoumba Mungu, cha muhimu zaidi ni nini?
-Wanadamu.

-Kwa sababu wanadamu walikuwa wa muhimu zaidi ya kila kitu ambacho Mungu aliumba, je Mungu aliamua kutuumba vipi?

-Mungu aliamua kutuumba kwa mfano wake.

-Mungu aliumbaje wanadamu tofauti na wanyama?

-Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake, lakini wanyama

hawana mfano wa Mungu.

-Inamaanisha nini kusema binadamu waliumbwa kwa mfano wa Mungu?

-Haimaanishi miili yetu kwa sababu Mungu hana mwili wa nyama na mifupa.

-Sehemu yetu ambayo iliumbwa kwa mfano wa Mungu ni sehemu ambayo haiwezi kuonekana.

-Sehemu yetu ambayo iliumbwa kwa mfano wa Mungu ni nafsi yetu.

-Nafsi zetu zina sehemu tatu.

-Kwa nafsi zetu, kuna akili, hisia na mapenzi.

-Akili yetu, hisia, na mapenzi vyote viliumbwa kwa mfano wa Mungu.

-Ni sehemu ipi ya wanadamu iliyoumba kwa mfano wa Mungu?

-Akili, hisia na mapenzi yetu.

-Kwanza Mungu aliumba akili zetu kwa mfano wake.
-Kwa sababu Mungu ana akili, alituumba na akili pia.

-Mungu anafikiria na anatutaka tufikirie pia.



-Mungu anataka tufanye nini na akili yetu?

-Mungu anatutaka tufikirie kilicho kizuri.
-Mungu anatutaka tumfikirie yeye.

-Mungu anataka tufikirie kumhusu ili tumjue.

-Ungependa kuishi kichakani na wanyama pasipo watu?
-La.

-Kwa nini?
-Kwa sababu wanyama hawawezi kuongea na kufikiri.

-Kama vile mnavyo ongea na marafiki wenu, Mungu pia anatutaka tuongee na yeye.

-Mungu ana akili na alituumba pia na akili.
-Mungu ametupa akili ili tumjue yeye.

-Pili Mungu aliumba hisia zetu kwa mfano wake.

-Kwa sababu Mungu ana hisia, alituumba na hisia pia.

-Mungu hufurahi na anatutaka tuwe na furaha.

-Mungu anatutaka tuwe na furaha kumhusu.
-Mungu anatutaka tumpende yeye.

-Mungu pia anachukia.

-Mungu anachukia nini?
-Mungu anachukia dhambi zote.

-Dhambi ni nini?

-Dhambi ni kile ambacho Mungu hataki.
-Dhambi ni kila kitu ambacho Mungu hataki.

-Mungu pia huuzunika.

-Mungu huuzunishwa na nini?
-Mungu huuzunishwa na watu ambao hawampendi.

-Kama vile muwapendavyo watoto wenu, Mungu anawapenda pia.

-Mungu ana hisia na alituumba na hisia.

-Kwa nini Mungu akatupatia hisia?
-Ili tumpende Mungu.

-Tatu, Mungu aliumba na mapenzi  kwa mfano wake.

-Kwa sababu Mungu ana mapenzi, alituumba na mapenzi.

-Mungu anaweza kuchagua, na anatutaka tuchague pia.

-Mungu anataka tufanye nini na mapenzi yetu?

-Mungu anatutaka tuchague kile kilicho kizuri.



-Mungu anataka tumchague yeye.

-Mungu anataka tumchague ili maisha yetu yawe mazuri.

-Ukifyatua bunduki, je bunduki inachagua kitu cha kulenga?
-La.

-Kwa nini?
-Kwa sababu buduki haina mapenzi yake.

-Ukiendesha mashua majini, je inachagua mahali pa kuelekea?
-La.

-Kwa nini?
-Kwa sababu mashua haina mapenzi yake.

-Mungu ana nia na alituumba na mapenzi.

-Mungu ametupa mapenzi ili tumchague yeye.

-Tusome kuhusu Mungu akimuumba binadamu wa kwanza:

Tusome Mwanzo 1:27

27-Basi, Mungu akaumba mtu kwa mfano wake; naam, kwa mfano wake Mungu alimuumba.  Aliwaumba mwanamume na mwanamke.

-Hapo mwanzo, Mungu aliwaumba watu wangapi?

-Mwanamume mmoja na mwanamke mmoja pekee.

-Kwanza, Mungu alimuumba mwanamume wa kwanza.
-Kisha, Mungu akamuumba mwanamke wa kwanza.

-Jina la mwanamume wa kwanza ni lipi?
-Adamu.

-Ni nani pekee aliyeweza kuumba mwanamume na mwanamke wa kwanza?

-Mungu pekee.
-Mungu pekee ana uwezo wa kuumba watu.

Tusome Mwanzo 2:7a

7-Basi, BWANA Mungu akamfanya mwanamume kwa mavumbi ya udongo.

-Mungu alimuumba Adamu kwa mavumbi ya udongo.

-Lakini kwa nini Adamu hakuwa hai?

-Kwa sababu Mungu hakuwa amempulizia Adamu pumzi ya uhai.

Tusome Mwanzo 2:7b

7-BWANA Mungu akampulizia puani pumzi ya uhai, na huyo mwanamume akawa kiumbe hai.



-Adamu alikuwa hai wakati Mungu alipompulizia pumzi ya uhai.

-Mungu pekee anaweza pulizia watu pumzi ya uhai.
-Mungu pekee ndiye wa kupeana uhai.

-Adamu ndiye wa kwanza kwa vizazi vyote vya wanadamu.
-Adamu ndiye baba wa kizazi chote cha wanadamu

-Hapo mwanzo Mungu hakuumba mzungu na mtu mweusi.

-Hapo mwanzo Mungu alimuumba mwanamume mmoja na mwanamke mmoja.

-Watu wote wanatoka kwa Adamu.
-Watu wote ni kizazi cha Adamu.

-Baada ya Mungu kumuumba Adamu, alimfanyia nini?

Tusome Mwanzo 1:28

28-Mungu akawabariki na kuwaambia, “Zaeni muongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki; muwatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, na kila kiumbe hai kitembeacho duniani.”

-Mungu alimpa Adamu mamlaka juu ya nchi.

-Kwa nini malaika hawana mamlaka juu ya nchi?

-Kwa sababu Mungu aliwaumba wanadamu wawe na mamlaka juu ya nchi.

-Kwa nini mapepo hawana mamlaka juu ya nchi?

-Kwa sababu Mungu aliwaumba wanadamu wawe na mamlaka juu ya nchi.

-Nani aliyeumba nchi?
-Mungu.

-Nchi ilikuwa ya nani?
-Mungu.

-Ulikuwa uamuzi wa nani kuwafanya wanadamu kuwa na mamlaka juu ya nchi?

-Wa Mungu pekee.

-Mungu alisema nini baada ya kuumba vitu vyote?

Tusome Mwanzo 1:31

31-Mungu akaona kila kitu alichokifanya kuwa ni chema kabisa.  Ikawa jioni, ikawa asubuhi; siku ya sita.

-Baada ya Mungu kuumba vitu vyote, aliviona kuwa ni vizuri.

-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu, kila kitu Mungu aliumba ni kikamilifu.



-Hapo mwanzo, maisha yalikuwa namna gani?

-Hapo mwanzo, hapakukuwa na hasira.
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na chuki.

-Hapo mwanzo, hapakukuwa na uovu.
-Hapo mwanzo, hapakukuwa na kifo.

-Hapo mwanzo, Mungu aliumba kila kitu kikamilifu.

-Nani aliyekuwa akitazama wakati Mungu aliumba dunia kamilifu?

-Malaika wa Mungu, Shetani, na mapepo wake.

-Malaika wa Mungu waliona ya kuwa Mungu aliumba vitu vyote vikamilifu.

-Walikuwa na furaha.

-Je, Shetani na mapepo wake walifurahi kwa sababu Mungu aliumba dunia kamilifu?
-La.

-Shetani na mapepo wake waliona ya kuwa Mungu aliviumba vitu vyote vikamilifu na wakawa na hasira sana.

-Shetani na mapepo wake waliona ya kuwa Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake na wakawa na hasira sana.